MWONGOZO

KARATASI YA PILI

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

## UFAHAMU

1. *Ipe taarifa hii kichwa mwafaka.* *(alama 1)*

   ***UCHAFUZI WA MAZINGIRA***

   ***ZIWA NAKURU***

2. *Eleza sababu zinazofanya Ziwa Nakuru kuchafuka.* *(alama 2)*

   **a. *Maji taka kuingia mbugani***

   **b. *Miundo msingi duni***

3. *Ni nini madhara ya kuchafuliwa kwa Ziwa Nakuru?* *(alama 4)*

   **a. *Kuhama kwa ndege***

   **b. *Kuangamia kwa wanyama pori***

   **c. *Maradhi kadha kwa wanyama pori***

   **d. *Mkondo wa maji kuzibwa***

4. *Eleza vizingiti vinafanya ziwa hili kuendelea kuchafuliwa.* *(alama 2)*

   **a. *KWS kutokuwa na bajeti ya kusafisha mbuga***

   **b. *Utepetevu wa NEMA kwa kukosa kuweka sheria kali.***

5. *Toa mapendekezo yanayoweza kusaidia kumaliza uchafuzi wa Ziwa Nakuru kulingana na taarifa hii.* *(alama 4)*

   **a. *Baraza la mji kuhakikisha makazi ni safi***

   **b. *Baraza la mji kuzoa taka kutoka makazi ya watu***

   **c. *Wananchi kuhimizwa kupunguza matumizi ya vitu vya plastiki***

   **d. *Kuweka bajeti ya kusafisha mazingira***

6. *Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika taarifa.* *(alama 2)*

   *a. Kupenyeza*-***Kupita katikati***

   *b. Utepetevu* -***Ulegevu, uvivu***

# UFUPISHO

(a)

1. *Sekta ya kilimo inachangia asilimia 25 ya pato la taifa*
2. *Inatoa ajira kwa asilimia 40 ya wakenya*
3. *Huchangia asilimia 65 ya mapato yatokanayo na mauzo ya nje.*
4. *Hutegemewa na asilimia 80 ya wakenya kwa uhai*
5. *Kustawi kwake kutaimarisha uchumi*

*(Hoja 5 x 1 = alama 5)*

*(b)*


# UFUPISHO

(a)

1. Sekta ya kilimo inachangia asilimia 25 ya pato la taifa
2. Inatoa ajira kwa asilimia 40 ya wakenya
3. Huchangia asilimia 65 ya mapato yatokanayo na mauzo ya nje.
4. Hutegemewa na asilimia 80 ya wakenya kwa uhai
5. Kustawi kwake kutaimarisha uchumi

**(Hoja 5 x 1 = alama 5)**


(b)

1. Serikali inatekeleza maamuzi mengi katika kilimo
2. Mbinu za kuustiri umma zimepewa umbele.
3. Sera ya bei za bidhaa za kilimo zimeleta kushiriki kikamilifu na udhibiti wa serikali.
4. 2011 Kenya ilipanga kuongeza maradufu hifadhi ya nafaka
5. Serikali imeelekeza juhudi katika sekta ya kibiashara
6. Juhudi za kuhakikisha usalama wa chakula zimekuwepo/zimetekelezwa.
7. Serikali imekuwa ikiongeza hisa inayotengewa Wizara ya Kilimo katika makadirio yake.

**(zozote 7 x 1 = 07)**

M **Swali a. – alama 5** **S** – 6 x ½ = 03

**Swali b. – alama 7** **H** – 6 x ½ = 03

**M** – $^{3}/_{15}$ **Z** – maneno 10. 1z

3. **MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40)**

a) Taja ala zinazotumika kutamkia sauti /ch/ (alama 1)

½ ½

Kaakaa gumu na Baba la ulimi.

b) Tunga sentensi moja ukitumia nomino na kielezi kutokana na neno: enda (alama 2)

Nomino ⇒ Mwendo, Kuenda Kielezi : Nilimpata Mwendoni

E

c) Tunga sentensi ukitumia nomino katika ngeli ya 'U-YA' ili kuonyesha upatanisho wa kisarufi

(alama 2)

Ugonjwa huo umehatarisha maisha.

Magonjwa hayo yamehatarisha maisha.

d) Eleza tofauti za sentensi hizi. (alama 2)

i. Nilimpata huku. Pahala pasipo (1) dhahiri.

ii. Nilimpata humu. Pahala palipo (1) dhahiri. (undani)

e) Onyesha matumizi ya kiambishi 'ji' katika sentensi ifuatayo:
Mkiambiaji alijibidiisha katika riadha (alama 2)

M.Kimbiaji ⇒ Mtendaji (1)

alijibidiisha ⇒ Kirejeshi cha mtenda. (1)

f) Tumia vitenzi vifuatavyo kutunga sentensi katika kauli ya kutendeka

(i) Cha (alama 1)

Atumie

cheka (1) au shika (1) Mtoto hakukubali kuachika haraka na mamake.

(ii) Pa (alama 1)

Atumie

(Peka) Pesa si kitu kinachopeka vivi hivi.

g) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao KN(N) + KT (t + T + E) (alama 1)

KN (N) + KT (t + T + E)

Maji yangali yanamwagika mtaroni

h) Tumia neno *'Kama'* katika sentensi kama; (alama 2)

i. Kitenzi

Mfugaji anakama ng'ombe.

ii. Kihusishi

Alikuka kama Marai.

① Utakula wali au ugali?

i) Tunga sentensi moja ukitumia kiunganishi cha uteuzi (alama 2)

au / ama (+1)

j) i) Kirai ni nini? (alama 1)

Neno au fungu la maneno ambalo halina muundo wa KN na KT hivyo hakina maana kamili.


ii) Onyesha aina ya virai katika sentensi ifuatayo.
Mwaka juzi alikwenda ulaya (alama 2)

KN/RN → Mwaka juzi; RT → alikwenda ulaya

k) Kwa kutoa mfano mmoja wa sentensi eleza maana ya shamirisho kitondo (alama 2)

Ni nomino inayotendewa kitendo au inayonufaika kutokana na utendaji wa kitendo.

l) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi: (alama 4)
Ule mkongojo wa babu ulinunuliwa na fundi




Ondoa nusu alama kwa kila kosa

m) Tunga sentensi moja ukitumia vitate hivi: (alama 3)

(i) Kipofu

(ii) Kibovu

(iii) Kibofu

Kipofu mwenye kibofu kibovu ametibiwa

Kipofu: Mtu asiye na uwezo wa kuona.
Kibovu: Kibaya//Kilichooza//isiyofaa
Kibofu: Mpira unaotiwa upepo ili kuchezewa na watoto (Baluni)

n) Eleza mofimu zilizomo katika neno hili. (alama 3)
Lililolila

Li - li - lo - li - l - a

(i)
Li – Ngeli
Li – wakati uliopita
Lo – Kirejeshi
Li – yambwa tendwa
l – mzizi
a – Kiishio

(ii) −½

o) Tunga sentensi moja ukitumia kihisishi cha masikitiko. (alama 2)

Yarabi! Mola amlaze pema

1×2 = 2

p) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya alama ya kibainishi. (alama 2)

Ng'ombe/ chelang'at

1×2 = 2 Sentensi Kibainishi

q) Andika katika usemi wa taarifa
"Utaweza kuwa mwindaji mashuhuri ikiwa utayafuata mashauri yangu," alisema mbunda. (alama 2)

Mbunda alisema kuwa angeweza kuwa mwindaji mashuhuri ikiwa/kama angeyafuata mashauri yake.

−½

r) Tunga sentensi ukitumia kinyume cha kitenzi hiki: Ezeka (alama 2)

Ezua// Wajenzi waliezua paa la nyumba.

s) Yakinisha sentensi ifuatayo:
Tusingalienda hospitali, tusingalitibiwa. (alama 1)

Tungalienda hospitali tungalitibiwa. −½

4. **ISIMU JAMII: (ALAMA 10)**

a) Fafanua istilahi zifuatazo za isimu jamii (alama 2)
(i) Isimu

Sayansi inayochunguza matumizi ya lugha.

(ii) Jamii

Kundi la watu wenye uhusiano na maingiliano mbalimbali.
Kundi la wetu wenye uhusiano wa aina fulan

b) "......ah.....naomba kumwongelesha Chucho.....Naam, naam Chucho.......Hujambo? .....si.....sina neno......naam. Mjomba amezidiwa si wa maji si wa chakula....kweli?......Muuguzi mkuu amedhihirisha..... Yes......ok......yeah.....Ala! Ameishiwa na pesa.

(i) Tambua sajili husika katika dondoo hili. (alama 1)

Sajili ya simu / Rununu / simu tamba.

(ii) Kwa hoja zozote saba, eleza sifa za sajili hii. (alama 7)

i) Hutumia sentensi fupi fupi.
ii) Kuna matumizi ya maswali na majibu.
iii) Hutumia takriri: Chucho, naam.
iv) Huhusisha kuchanganya ndimi.
v) Kanuni za kisarufi hukiukwa.
vi) Hulenga moja kwa moja kiini cha habari.
vii) Kuna kukatizana kalima. ...
(viii) Kuna maamkizi.

**KILA LA HERI !!**

© 2020